


DHULUMA DHIDI YA WATU WEUSI KATIKA HADITHI FUPI TEULE

Na

David Wang'ara Mbatia



**Shule ya Sayansi za Kijamii
(Idara ya Lugha)**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya
Uzamili katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya.**

FEBRUARI, 2014

IKISIRI

Utafiti huu huu umetathmini suala la dhuluma dhidi ya watu weusi katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Mtafiti ametumia hadithi fupi nne kutoka kwa diwani nne za hadithi fupi. 'Weusi Huu' (Ken Walibora , 2006) Katika *Diwani ya Maskini Milionea na Hadithi nyingine*, 'Hajiri Ahajiri' (Omar Babu, 2006) Kwenye Diwani ya *Maskini Milionea na Hadithi nyingine*. 'Damu Nyeusi' (Ken Walibora ,2006) Katika Diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*. 'Kunani Marekani' (Iribe Mwangi, 2007) Katika Diwani ya *Kunani Marekani na Hadithi nyingine*. Mtafiti amelenga kuchunguza jinsi waandishi wa hadithi fupi teule zilizomo kwenye diwani hizi walivyoshughulikia suala la dhuluma dhidi ya watu weusi. Kwa kuchunguza asasi ambazo huendeleza dhuluma dhidi ya watu weusi, sababu na matokeo ya dhuluma kwa mujibu wa hadithi zitakazoteuliwa. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Ubaguzi. Nadharia hii inaeleza kuwa kuna vigezo fulani ambavyo wabaguzi hutumia katika huwabagua watu wa kundi fulani. Tasnifu hii la imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa suala la utafiti, sababu za kuchagua, malengo ya utafiti na misingi ya nadharia. Sura ya pili, imeshughulikia yalioandikwa kuhusu mada hii. Katika sura hii historia na maendeleo katika hadithi fupi yameonyeshwa. Aidha , mtafiti ametathmini maandishi mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Sura ya tatu, imeshughulikia mbinu zilizotumiwa ili kufanikisha utafiti huu. Sura ya nne, imeangazia aina mbalimbali za dhuluma za kibaguzi zinazotekelezwa dhidi ya watu weusi kwa mujibu wa hadithi fupi zilizoteuliwa. Aidha, mtafiti katika sura hii ametathmini ufanisi wa waandishi wa hadithi fupi teule katika kusawiri maudhui ya dhuluma za kibaguzi. Sura ya tano, imejikita katika hitimisho na muhtasari wa sura zote pamoja na mapendekezo ya tafiti za baadaye.